

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA AROBAINI NA NNE

16 JUNI, 2016



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA AROBAINI NA NNE – 16 JUNI, 2016

I. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:

II. MASWALI YA KAWAIDA:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

374. MHESHIMIWA BONIPHACE MWITA GETERE (BUNDA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Malambo ya Kijiji cha Mikomahiro, Salamakati, Salama A, Sanzati, Mgeta, Kihumu/Hunyari na Nyang'aranga yamekuwa hayatumiki ipasavyo kutokana na magugu maji na hivyo kujaa matope:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha malambo haya ili yatoe huduma nzuri kwa watumiaji;

(b) Malambo haya yalichimbwa miaka ya nyuma na watumiaji kwa sasa wameongezeka; Je, Serikali ina mpango wa kuyapanua malambo hayo ili kukidhi mahitaji ya watumiaji kwa sasa.

WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

375. MHESHIMIWA HASANI SELEMAN KAUNJE (LINDI MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:- Kuna migogoro ya ardhi iliyosababishwa na upimaji na ugawaji wa ardhi kwa ajili ya makazi na ujenzi wa Taasisi katika Kata ya Rasbura eneo la Mitwero. Aidha, watumishi wa Idara ya Ardhi walijigawia ardhi kinyume na taratibu na kuviuza kwa manufaa yao. Pia wananchi wanalalamikia fidia na utwaaji wa maeneo makubwa tofauti na michoro iliyomo kwenye nyaraka zilizothibitishwa na Wizara kwa matumizi ya Taasisi za Umma au binafsi:-

Je, Serikali ipo tayari kufanya uchunguzi au uhakiki wa zoezi zima la upimaji na ugawaji wa viwanja katika eneo hilo.

WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:

376. MHESHIMIWA JOSEPH OSMUND MBILINYI (MBEYA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:-

Je, ni lini jengo jipya la maabara ya mionzi linalojengwa kwa muda mrefu sasa kwenye Hospitali ya Rufaa ya Mbeya litakamilika na vipimo vya CT Scan na MRI Scan vitaletwa na kuanza kazi.

WIZARA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:

377. MHESHIMIWA AMINA NASSORO MAKILLAGI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi:- Zao la Mwani limekuwa ni ukombozi kwa vikundi vya akina mama katika mwambao wa Pwani:-

(a) Ni lini Serikali itavipatia mtaji vikundi vya wanawake wa kilimo cha Mwani ili kuongeza uzalishaji kutoka tani 12,000 hadi 20,000 kwa mwaka;

(b) Ni lini Serikali itawapatia Nyezo na Utaalam ili vikundi vya wanawake na vijana viweze kuzalisha Chaza, Walulu, Kaa, Kamba na Pweza.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI:

378. MHESHIMIWA RAISA ABDALLAH MUSSA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi:- Mfumo wa elimu ya Tanzania kwa kiasi kikubwa haumwandai mwanafunzi kuwa mbunifu na kuweza kujiajiri:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kubadili mfumo wetu wa elimu ili kuchochea mwanafunzi kuwa mbunifu na kuwa na uwezo wa kujiajiri;

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha mtaala wa elimu utakaotoa mafunzo yanayozalisha ajira.

III. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

(Kusomwa Mara ya Kwanza)

Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Ununuzi wa Umma wa Mwaka 2016 [*The Public Procurement (Amendment) Bill, 2016*].

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Kwamba, Bunge likubali kujadili Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2015 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

Kwamba, Bunge likubali kupitisha Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
16 JUNI, 2016**

**DKT. T. D. KASHILILAH
KATIBU WA BUNGE**